

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA**

**SHULE YA SEKONDARI MINEPA  
S.L.P 156,  
MAHENGE/ULANGA  
...../...../20.....**

KUMB.Na.MNSS/JOI/VOL I .....  
**JINA LA MWANAFUNZI**

S.L.P.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA  
SEKONDARI MINEPA WILAYA YA ULANGA MKOA WA MOROGORO MWAKA .....**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka ..... Shule ya Sekondari ya Minepa ipo umbali wa km 65 kaskazini mwa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ..... saa moja asubuhi  
Unatakiwa kuripoti Shule kuanzia tarehe.....saa moja asubuhi na mwisho wa kuripoti ni tarehe.....

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE YA SHULE**

Sare ya Shule hii ni kama ifuatavyo:-

- i. Wasichana sketi mbili
- ii. Wavulana suruali mbili vipimo pindo la chini la suruali liwe na upana usiopungua inchi 16 na usiozidi inchi 20.
- iii. Rangi ya kitambaa kwa sketi na suruali ni ya kaki sampuli ya kitambaa imeambatanishwa pamoja na fomu hii.
- iv. Mashati meupe mawili mawili ya mikono mifupi
- v. Fulana (T-Shirt) ya dark bluu yenyenembo ya shule
- vi. Viatu vya ngozi nyeusi vya kufunga na kamba visiwe na kisigino kirefu
- vii. Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana
- viii. Tai ndefu ya rangi ya kaki
- ix. Rangi ya hijabu ifanane na sare za shule.

**ANGALIZO**

Ukionekana umeavaa suruali yenyenembo au tofauti na mshono wa shule pamoja na T- sheti isiyo sahihi hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako ikiwemo kuingia gharama nyingine ya mashono ya nguo mpya.

**2.3 SARE ZA MICHEZO KWA SHULE HII NI :-**

- i. Wavulana traki suti ya bluu, pamoja na fulana (T-shirt) ya bluu
- ii. Wasichana traki suit ya bluu,bukta,pamoja na fulana (T-shirt) ya bluu.

## **2.4 VIFAA VYA DARASANI**

- i. Daftari 10 aina ya msomi na 10 aina ya kaunta buku
- ii. Mkebe, rula na flat file
- iii. Begi la kuhifadhia /kubebea daftari zake.
- iv. Passport size ( picha zitapigwa shulen i kwa malipo) picha hizo zitatumika kwa kazi maalumu.

## **2.5 CHAKULA NA MATIBABU**

Kutakuwa na mchango wa chakula cha mchana utakaoratibiwa na kamati ya wazazi walezi wenyewe kwa kushirikiana na Afisa Elimu Kata.

## **2.6 VIFAA VYA USAFI**

Usafi wa mazingira ya shule unatakiwa kufanyika kila siku na wanafunzi wenyewe kwa kuwa usafi ni sehemu ya elimu kwa vitendo au elimu ya kujitegemea hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shulen i vifaa vya usafi kama vile jembe lenye mpini.fyekeo/kwanja, ndoo ndogo ya lita kumi n.k. Ili kumpunguzia usumbufu mwanafunzi na kuleta ufanisi kwa kazi vifaa hivyo vitapokelewa na kuhifadhiwa shulen na kutumika pindi vitakavyo hitajika kadri ratiba ya usafi na elimua ya kujitegemea itakavyo pangwa.

## **2.7 HITIMISHO**

Uongozi wa shule na jumuiya ya Minepa Sekondari inakukaribisha ili upate haki yako ya msingi ya kupata elimu.

Utakapofika shulen i utapewa na kuelekezwa sheria za shule ambazo katika kipindi chote utakapofika shulen i utatakiwa kuzifuata, kuzitij na kuziheshimu,kinyume na hapo utapewa adhabu kali ikiwa pamoja na kufukuzwa shule.


**"KUMBUKA KWAMBA ELIMU NI UFUNGUO WA MAISHA HIVYO MZAZI AU  
MLEZI HAKIKISHA UNAMLETA MWANAO SHULENI SIKU ILIYO PANGWA  
KINYUME NA HAPA HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI  
YAKO KWANI KUMNYIMA MTOTO HAKI YAKE NI KOSA LA JINAI.**

Ufikapo shulen i ripoti Ofisini kwa mkuu wa shule ili usajiliwe

**TANBIHI:-** Siku ya kufungua shule ni lazima uje na mzazi/mlezi wako kinyume na hapo hutapokelewa.

Karibu sana Minepa Sekondari kauli mbiu yetu.

**"MOTTO WETU" EDUCATION FOR SERVICE**

  
.....

**SOSTHENES E. LIYOWELA**

**MKUU WA SHULE**

**MINEPA SEKONDARI**  
**S. L. P. 156**  
**MAHENGE/ULANGA**